**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

Simu +025 2552693
Nukushi + 025 2552586
Barua Pepe ded@rungwedc.go.tz
Tovuti www@rungwedc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe,
2 barabara ya Halmashauri
Tukuyu Sekondari,
S.L.P. 148,
**53582 Rungwe,**
**MBEYA.**

Tarehe: 03/01/2025

**Kumb. Na.RDC/C6/122/VOLIV/128**

MKURUGENZI MKUU,

BODI YA CHAI TANZANIA,

S.L.P 2663,

**DAR ES SALAAM.**

**YAH: OMBI LA ENEO LENYE UKUBWA WA HEKTA TATU (3) KWA AJILI YA KUJENGA VIWANDA VYA KUCHAKATA NA KUFUNGASHA CHAI, OFISI NA NYUMBA ZA WAFANYAKAZI**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo.

2. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Rungwe inakiri kupokea barua toka Ofisi yako ya tarehe 27 Desemba, 2024 yenye **Kumb. Na. AD.68/264/01/12** ambayo ilikuwa na kichwa cha habari tajwa hapo juu.

3. Pamoja na barua tuliyokuandikia yenye **Kumb. Na.RDC/C6/122/VOLIV/127** ya tarehe 24/12/2024 kama inavyohusika, tunanaomba vielelezo vifuatavyo viwasilishwe kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Rungwe haraka iwezekanavyo ili viweze kuridhiwa vikao vyote vya kisheria kwa ajili ya hatua zaidi za utekelezaji.

   i. Jina la kampuni linalotaka kuwekeza

   ii. Andiko la mradi

iii. Cheti cha usajili wa kampuni toka BRELA na *Memorandum and Article of Association*

iv. Barua toka TIC

v. Nyaraka zingine muhimu zinazoweza kusaidia uwekezaji wa kiwanda

4. Kwa barua hii, Halmashauri inaridhia ombi lako. Aidha, Halmashauri ya Rungwe ina eneo lingine lililopo Kata ya Nkunga Kijiji cha Nkunga lenye ukubwa wa ekari saba (7) ambalo Halmashauri inashughulikia upatikanaji wa ramani yake. Pamoja na barua hii, naambatanisha ramani ya eneo lililopo katika Kata ya Kyimo Kitongoji cha Ilenge lenye ukubwa wa mita za mraba 17,047 ambazo sawa na hekta 1.7047.

5. Nakutakia utekelezaji mwema.

Feliche Kigava

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**RUNGWE**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE

**Nakala:**

Katibu Mkuu,
Wizara ya Kilimo,
Idara ya Utawala,
Mji wa Serikali Mtumba,
S.L.P 2182,
**40487 DODOMA**

Katibu Tawala Mkoa,
Mkoa wa Mbeya,
S.L.P 754,
**MBEYA.**

Katibu Tawala Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe,
S.L.P 34,
**TUKUYU.**

**ENEO LA UWEKEZAJI LILILOPO ILENGE**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

